

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULIZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI

27 MEI, 2016



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI – TAREHE 27 MEI, 2016

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

II. MASWALI:

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

249. MHESHIMIWA JAMAL KASSIMU ALI (MAGOMENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Serikali katika kipindi hiki imejipanga kufufua viwanda vyetu:-

Je, katika mipango hiyo mizuri Serikali imejipanga vipi kusaidia wananchi kuweza kuanzisha viwanda hivyo.

**250. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS GULAMALI
(MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:-

- (a) Je, ni lini Serikali itakwenda kuona hali ya kiwanda cha Manonga na kukifanya kiweze kufanya kazi na kutoa ajira kwa vijana wa Mkoa wa Tabora;
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kukiangalia upya kiwanda cha Nyuzi Tabora ili uzalishaji uweze kuanza.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

**251. MHESHIMIWA SUSAN CHOGISASI
MGONOKULIMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali imeshalipa stahiki za wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

252. MHESHIMIWA LAMECK OKAMBO AIRO (RORYA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Usambazaji wa umeme kupitia REA ulikusudiwa kufikishwa kwenye Vijiji na senta 54 kwenye awamu ya pili na ingewezesha upatikanaji wa umeme asilimia 25 - 30, kwani upatikanaji wa umeme kabla ya mpango huo ulikuwa ni asilimia 5 na kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya umeme kwa maendeleo ya wananchi wa Rorya umeme wa asilimia 25 bado ni wa chini sana na hata hivyo bado mradi unasuasua:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kasi ya usambazaji umeme katika Wilaya ya Rorya;
- (b) Je, ni lini mpango wa REA utakamilika na kuanza REA III;
- (c) Je, REA III ina Vijiji na senta ngapi ndani ya Wilaya ya Rorya.

**253. MHESHIMIWA EZEKIEL MAGOLYO MAIGE
(MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Kilio kikubwa cha wananchi waishio jirani na mgodi wa Bulyankulu ni kunufaika na mgodi huo:-

- (a) Je, ni kiasi gani cha pesa mgodi wa Bulyankulu ulitumia katika miradi ya ujirani mwema;
- (b) Je, kwa nini mgodi huo hautekelezi miradi yake kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ambako kuna wataalamu na gharama za utekelezaji miradi ni ndogo.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO:**

254. MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (KAWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Serikali iliwaahidi wananchi wa Jimbo la Kawe kujenga kwa kiwango cha Lami barabara ya Chuo Kikuu cha Ardhi - Makongo - Goba na barabara ya Tegeta Kibaoni - Wazo Hill - Madale:-

Je, ni lini ujenzi huo utakamilika.

**255. MHESHIMIWA ABDALLAH ALLY MTOLEA
(TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Ili Watanzania wanufaike katika ajira zinazotokana na shughuli za uchimbaji wa gesi na mafuta wanatakiwa kuwa na cheti cha *Basic Off Shore Safety Certificate* ambacho kwa sasa hakipatikani katika vyuo vya hapa nchini:-

Je, ni lini Serikali itakiwezesha Chuo cha DMI (*Dar es Salaam Marine Institute*) ili kianze kutoa kozi hii ili wananchi wote waweze kupata cheti hiki ili waweze kuajiriwa katika shughuli za gesi na mafuta.

**256. MHESHIMIWA JUMAA HAMIDU AWESO
(PANGANI)**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Ujenzi wa barabara ya Tanga - Pangani - Saadani yenye km 178 kwa kiwango cha lami ni ahadi ya muda mrefu ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na Rais wa Awamu ya Tano:-

Je, ni lini ujenzi huo utaanza hasa ikizingatiwa kuwa ahadi hiyo ni ya muda mrefu.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

(Majadiliano yanaendelea)



**DODOMA
27 MEI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**